**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dar es Salaam***
***24 Mei, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni katika hafla iliyofanyika Ikulu.

Viongozi walioapishwa ni Prof. Tumaini Joseph Nagu aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia masuala ya afya; Dkt. Blandina Buganzi Kilama aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango anayeshughulikia biashara na ubunifu; na Jaji Mstaafu John Samweli Mgetta aliyeteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Maadili.

Akizungumza katika hafla hiyo, Rais Dkt. Samia aliwataka viongozi wateule kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu, huku wakishirikiana kikamilifu na watumishi watakaowakuta katika maeneo yao ya kazi.

Vilevile, Rais Dkt. Samia aliwasisitiza viongozi hao kuviishi viapo vyao kwa vitendo, wakizingatia nidhamu, maadili na uzalendo katika utumishi wa umma na kuwa mfano wa kuigwa katika uongozi bora na uwajibikaji kwa maendeleo ya Taifa.

Katika hatua nyingine, viongozi hao walikula kiapo cha maadili katika utumishi wa umma, wakiambatana na viongozi wengine wateule ambao ni Dkt. Fred Matola Msemwa, aliyeteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango; Ndugu Lazaro Jacob Twange, aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO); na Ndugu Thadei Aldo Kabonge, aliyeteuliwa kuwa Msaidizi wa Katibu wa Baraza la Mawaziri.

Shaaban Kissu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu